

COMPANY HIGHLIGHT

# Miaka Ishirini na Sita KVTC

Na Leslie Mascarenhas

## Tanwat & DPSO

Nilijiunga na kampuni ya Miwati Tanganyika (TANWAT) 1974 katika ofisi ya Dar Es Salaam. Baba yangu alijiunga na TANWAT 1973 na kufungua ofisi ya TANWAT Dar Es Salaam na baadae nilikuja kuungana nae katika ofisi ya usaidizi wa Mradi Dar ("DPSO").

Wakati huo meli za makontena hazikuwepo. Magunia yalikuwa yanapakiwa kwa mkono kwenye magari na kupelekwa bandarini kwa kusafirishwa kwa meli.Mawasiliano na wateja kwa huduma ya telegram na maandiko yote yalifanywa kwa mashine za kuchapa.

## KVTC Kujitegemea

1992 wakati CDC ilipoanza kuwekeza KVTC kampuni ilisaidiwa kupitia DPSO hii ilimaanisha kuwa nilikuwa naangalia kampuni mbili KVTC na TANWAT.

2008 KVTC imekuwa kufikia shughuli za kibiashara na nikajiunga na KVTC peke yake kusaidia kukua kwa shughuli.

## Uchache wa makontena elfu

2009, KVTC ilianza kusafirisha nje mbao za mitiki kutoka kwenye kiwanda chake cha kuchakata mbao. Kwa miaka, tumesafirisha kiasi cha 80,000m3 ya mbao kutoka KVTC zote zimepakiwa kwenye makontena (>3000 20's na 40's!!) na maandiko yote yanaandaliwa na kompyuta na kupelekwa kwa barua pepe.

Ilikuwa ni safari ya kuvutia kushuhudiwa mabadiliko na jinsi gani teknolojia ilivyo fanya maisha yetu yawe mepesi zaidi lakini wakati huohuo imeleta msukumo zaidi na imeongeza mahitaji kutoka kwa wateja na watoa huduma.

## Kustaafu na Makabidhiano

Baada ya miaka arubaini na nne kati ya hiyo ishirini na sita KVTC, kusaidia usafirishaji wa nje unaohusiana na shughuli za kampuni, wakati umefika wa kujiandaa na maisha baada ya KVTC na mwisho wa mwaka huu nitastaafu.

KVTC kwa sasa inafanya maandalizi ya kipindi cha mpwito na kuondoka, tumemuajiri mfanyakazi mwingine kwenye timu yetu, Arlene Gomes, kuni rithi nafasi yangu kuanzia Disemba mwaka huu.

## Nini kitafuata?

Natarajia mbeleni kutumia mda wangu na familia, kutembelea ndugu zangu India na Kanada lakini itakuwa kitu kigeni kutoenda ofisini kila siku. Ilikuwa ni furaha kufanya kazi na KVTC naitakia kampuni mafanikio yote huku mbeleni.

HIGHLIGHTS




## Woodmizer & KVTC

Kiwanda cha KVTC kina misumeno mingi kwenye msitari WA Titan uliotengenezwa na Woodmizer. Katika ziara yao ya kutathmini msitari, walitengeneza video ndogo

Kiwanda kimekata 265,000 cubic mita za ujazo kuanzia 2009 na inaendelea kuwa na nguvu. Iangalie hapa kwetu LinkedIn mlisho.



## Zuri Zanzibar

KVTC imekuwa moja kati ya wa zabuni muhimu wa chanzo endelevu cha mitiki kwa hoteli mpya ya ZURI Zanzibar www.zurizanzibar.com

# Kutoka Dawati la Hans

Na Hans Lemm

Kama mvua zinavyo anza kuisha tunaweza kuangalia nyuma katika msimu mzuri sana, mvua za kwanza zilinyesha mwisho wa Oktoba na wakati naandika tumepata mvua nzuri zaidi 1,300 mm nabado tunategemea chache zaidi kuongezeka.

Mwaka huu tumepanda kiasi cha hekta 340 kuanza mzunguko wa pili katika ardhi yetu na hekta 250 ya upandaji mpya kwa wakulima wan je kulifanya eneo jumla kwa mpango wa kusaidia wakulima wan je ifikie hekta 1250, na kiasi cha wakulima 400 wanapata pembejeo, msaada wa kifedha na huduma za ugani.

Tumepanga kupumzisha, kuanzia kati ya April mpaka kati ya Mei wakati wa msimu wa mvua kubwa, lakini tutarudi katika kiwango cha juu cha shughuli kabla ya mwisho wa mwezi.

Maada yahii kijaridi iko wazi ni kuhusu zamani na mpya. Kila mwaka tuna watu wanajiunga na sisi na wakati mwingine tunahitaji kusema kwa heri kwa watu ambao walikuwa nasi kuanzia mwanzo(kabla kabisa sijajiunga na kazi hii). Moja wao ni Leslie Mascarenhas ambaye ametushirikisha baadhi ya safari yake na wewe na ameona na amekuwa sehemu ya mabadiliko ya KVTC kuanzia siku ya kwanza.

Tume farijika kuweza kuvutia vijana na wenye vipawa kutoka sehemu mbalimbali duniani na tunafurahi kwamba Vlad alijiunga na sisi. Vlad analeta mawazo mapya na uzoefu katika kazi anayovutiwa. Kama kampuni tunatakiwa kuendelea kujifunza, kubadilika, kujaribu ujuzi na uzoefu, ni muhimu kwa hili.





*KVTC ilishiriki maonesho ya Misitu ilioandaliwa na PFP iliyofanyika Mafinga Machi 19-23*

### KVTC BIOMASS CHALLENGE

Jumla ya maombi 12 yamepokelewa kwa ajiri ya Changamoto Matumizi ya Mabaki ya Uchanaji Mbao na timu ya KVTC na PFP wako wanatathmini mapendekezo. Tunategemea kuwakilisha mshindi katika jarida linalofuata

### JE UNAJUA?

Mzunguko wa shamba la mitiki mpaka uvune inatofautiana kuanzia miaka 20 hadi 80, kutegemeana na mpangilio ulioandaliwa na mameneja na matarajio ya kifedha ya wawekezaji

# Miezi sita KVTC

Na Vladislav Vejnovic

## Utangulizi

Jina langu ni Vlad na nimejiunga na kampuni ya Mitiki mapema Desemba iliopita nilipojiunga kampuni kama meneja mipango na utafiti niki mrithi Wessel Snyman.

Kabla sijajiunga KVTC nilifanya kazi sehemu tofauti Ulaya na Africa katika miradi mbalimbali ya kimataifa yote ikihusiana na misitu na mali asili. Ninapenda mipango na usimamizi wa misitu, misitu midogo Africa, mamlaka ya misitu na biashara ya kimataifa ya mbao.

## Mtazamo wangu wa Awali

Baada ya nusu mwaka Mavimba , nina mtazamo kamili, mathalani, ninavutiwa ugumu na aina kazi za misitu mashambani. Hii ni moja ya sababu kwa nini, kwa maoni yangu kiwango cha usimamizi wa misitu KVTC kiko juu kuliko kawaida. zaidi ya yeyote nilivutiwa pale nilipogundua KVTC vilevile inapanda miti na wakulima wadogo na kuwasaidia kukuza mashamba ya mitiki vizuri sana na kupata kipato cha kuridhisa.

## Mduara wa Mafunzo

Kuishi na kufanya kazi Mavimba ni tofauti kutoka kila kitu nilichofanya kabla. Nafurahia changemoto za siku hadi siku pande zote mbili ofisini na mashambani. Kutokana na ukweli kuwa natoka Ulaya ambako sayansi ya misitu ni tofauti na sayansi ya misitu Afrika.-miezi sita ya mwanzo imekuwa ni fundisho kubwa kwangu.

## Ninavyo Changia

Katika miezi inayokuja ninatarajia kupata uelewa wa sayansi ya misitu ya biashara KVTC na vile vile Tanzania. Pamoja na wafanyakazi wa misitu KVTC natarajia kutatua changamoto tunazokabiliana mashamba ya kupanda na kuboresha ufanisi wa mashamba ya mitiki.

### WASILIANA NASI

WASILIANA NASI AU TUANGALIE :
kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

PO Box 655, Ifakara, TZ

PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ

### TUSIKILIZE

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Kwenye Radio Pambazuko 89.5FM

Kila Ijumaa 01.30 jioni na kila Jumamosi 01.30 asubuhi